HOTUBA YA NDUGU WELLINGTON CHIBEBE, MKURUGENZI WA SHIRIKA LA KAZI DUNIANI (ILO) KWA NCHI ZA TANZANIA, KENYA, RWANDA, BURUNDI NA UGANDA SIKU YA AFYA NA USALAMA KAZINI JUMAPILI, APRILI 28, 2019 MBEYA, TANZANIA.

Mh. Jenesta Mhagama (MP) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu , Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu.

Mh. Antony Mavunde (MP) Naibu Waziri, kaz, ajira na watu wenye ulemavu.

Mh. Andrew Massawe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,Ajira, Shughuli za Bunge, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Nd. Albert Chalamila – Mkuu wa Mkoa wa Mbeya

Mama Khadija Mwenda – Mtendaji Mkuu OSHA

Dr. Aggrey Mlimuka –Mkurugenzi Mtendaji ATE

Dr, Yahya K. Msigwa – Katibu Mkuu, TUCTA

Washiriki na wafanyakazi

Waandishi wa habari

Itifaki imezingatiwa

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Ndugu. Wellington Chibebena kwa niaba yangu mimi mwenyewe ,nawaletea salamu kutoka shirika la kazi duniani tunapoadhimisha siku hii muhimu ya afya na usalama kazini tukiwa na kauli isemayo "**usalama na afya na mustakabali wa kazi kuelekea uchumi wa viwanda**".

Tunapoadhimisha miaka mia moja mwaka huu, ya kuanzishwa Shirika la Kazi Duniani (ILO), kulinda maisha ya afya ya wafanyakazi wote limekua suala la kupewa kipaumbele katika lengo zima la kuendeleza haki za kijamii na kazi zenye staha tukizingatia kuwa swala la usalama na afya kazini

linahusu haki za binadamu na ni sehemu moja wapo kuu ya ajenda ya maendeleo ya watu. kwa mwaka huu maadhimisho haya yanalenga katika kuangalia yaliyofanyika katika miaka hii mia moja katika kuboresha afya na usalama kazini na pia kuona jinsi ya kuendeleza juhudi hizi tukizingatia mabadiliko kwenye teknolojia , kuongezeka kwa idadi ya watu, maendeleo endelevu, mabadiliko ya hali ya hewa na mipango ya kazi.

Tangu mwaka 1919, maswala yanahusu afya na usalama kazini yalijumuishwa kwenye umuhimu wa kulianzisha Shirika la Kazi Duniani ili kuongeza uelewa na umuhimu wa kuwalinda wafanyakazi kutokana na hatari kwenye maeneo ya kazi. Hii limewezesha kuhakikisha kuwa kushughulikia maswala ya ajali kazini magonjwa yatokanayo na kazi na vifo inaendelea kupewa kipaumbele kama changamoto muhimu katika kuhakikisha kuwepo haki za kijamii maendeleo endelevu. ndiyo maana katika mkutano mkuu wa kwanza wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) mwaka 1919, uliofanyika Washington, Marekani, baadhi ya mikataba kuhusu afya na usalama kazini iliandaliwa na kupitishwa.

Ndugu. Mgeni rasmi na wageni waalikwa,

Wafanyakazi wapatao milioni mbili nukta sabini na nane (2.78m) ulimwenguni wanafariki kila mwaka kutokana na kuumia au magonjwa kazini.Wengi wao milioni mbili nukta nne (2.4m) ikiwa ni kutokana na magonjwa kazini. Pia wafanyakazi zaidi ya milioni miatatu na sabini na nne(374m) huathirika kutokana na ajali za kawaida kazini, ambazo nyingi zinazuilika.

Msongo wa mawazo utokanao na kazi na magonjwa yasiyoambukiza vimekua changamoto kubwa ulimwenguni kote. Pia wafanyakazi wengi hupata changamoto zitokanazo na kazi, hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa wafanyakazi hawa wanahudumiwa vya kutosha kwa kuzingatia mabadiliko yanayoendelea kutokea kwenye ulimwengu huu wa kazi.hapa naomba nimnukuu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani , Bw. Guy Ryder, alipokua akihutubia huko Urusi hivi karibuni kwenye wiki ya afya na usalama kazini kuwa , " Sio mazingira ya kazi peke yake yamebadilika kwa

muda huu , ila pia ni uasili wa athari zitokanazo na afya na usalama kazini na hii itaendelea kuwepo kwa baadae "

Ndugu. Mgeni rasmi na wageni waalikwa,

Wakati Shirika la Kazi Duniani linaendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zinahusu afya na usalama kazini kwa nyakati tofauti, uandaaji na uendelezaji wa mikataba inayohusu eneo hili umekua ukipewa kipaumbele katika shughuli mbalimbali za shirika . Kwa sasa pamoja na maazimio muhimu yaliyokwisha andaliwa kuna zaidi ya mikataba 40 (conventions and recommendations) yanahosu usalama na afya kazini inayohusika na kama mionzi, matumizi ya kemikali, saratani, kilimo, ukaguzi maeneo ya kazi,madini na kadhalika. zaidi ya mikataba hii, pia kuna miongozo na vitini vya mafunzo vinavyolenga kujenga utamaduni wa kuzuia athari mbalimbali kutokea mahala pa kazi.

Kwenye ulimwengu wa kazi unaondelea kubadilika mikataba hii inaendelea kuwa muhimu. Ni muhimu izingatie mabadiliko kwenye usalama na afya kazini na umuhimu wa kujenga na kusisitiza utamaduni ambamo haki ya mazingira salama ya kazi yanazingatiwa katika ngazi zote.

tukiangalia hali ya afya na usalama kazini kwa sasa ,ajali mahali pa kazi na magonjwa yatokanayo na kazi kunapelekea athari kubwa kwa wafanyakazi na familia zao , kiuchumi na kwenye maisha yao ya kila siku.

Guest of honors, ladies and gentlemen.

Tanzania as a member of ILO has achieved many milestones on OSH including the following:

a) Preparation of the nation OSH policy and subsidiary legislation and a strategy for its implementation.
b) Registration of workplace as an ongoing exercise.
c) Establishment of a national system for recording and notification of occupational accident and disease.
d) Establishment of the workers compensation fund (WCF).

We wish to commend the government for these positive steps and urge them to continue strengthening the inspection and enforcement systems which will ensure improved adherence to the regulatory framework and international norms.

The employees and workers should ensure full participation in building a culture of prevention on occupational safety and health at their respective workplace by better observing law, rules and regulation that would lower accident rates, and fewer work-related health problems.

We have no doubt that implementation of the above measure is key to ensuring better OSH environment in the future of work as the country transform into a semi-industrialized, middle income country

Nd. mgeni rasmi na wageni waalikwa,

Naomba kuchukua fursa hii pia kuipongeza serikali ya Tanzania ikifanya kazi kwa karibu na wadau mbali mbali kwenye swala la tatizo la ukimwi,kwa kuzindua kampeni kubwa ya upimaji wa ukimwi nchi nzima, ambayo ilizinduliwa na mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Juni mwaka jana ambayo inaendelea kuonyesha mafanikio makubwa.

Kufuatana na ripoti ya kamisheni ya ilo ya mustakabali wa kazi iliyozinduliwa Januari mwaka huu, tunaalikwa wote tutoe kipaumbele kwenye masuala ya utu katika uandaaji wa sera zinahusu kazi, ili kuhakikisha afya na usalama mahala pa kazi na pia kutambua eneo hili kama sehemu ya kanuni na haki ya msingi kwa wafanyakazi.

Tutumie fursa zilizopo ili tuweze kuandaa mustakabali wa kazi wenye kutuhakikishia afya na usalama mahala pa kazi kwa wote.

Muda wa kuchukua hatua ni sasa!